

G. Utekelezaji wa Kilimo cha Kitalu Nyumba Mkoa wa Ruvuma.

Mkoa wa Ruvuma umetekeleza ujenzi wa greenhouse (vitalu nyumba) vinane katika Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma na kutoa mafunzo ya ujenzi kwa vijana **20** kwa kila Halmashauri ni sawa na vijana **157** kwa Mkoa Mzima, na mafunzo ya uzalishaji wa mazao kwa vijana **100** kwa kila Halmashauri ni sawa na vijana **793** kwa Mkoa mzima,

Lengo la mradi

Kuwawezesha vijana kupata ujuzi kupitia kupitia mafunzo ya Kitalu Nyumba.

H. Malengo na Mpango wa Mkoa kupitia mradi huu;

- Kila Halmashauri kuendelea kutoa mafunzo kwa vijana **500** kila mwaka.
- kuwawezesha vijana, Wanawake na Wenye Ulemavu kupata mikopo kutoka asilimia 4,4 na 2 ili waanzishe miradi ya Kitalu Nyumba.
- Kuwaunganisha vijana waliopata mafunzo na taasisi za kifedha kama vile Tanzania Agricultural Development Bank (TADB) ili waweze kupata Mkopo wa kujenga mradi wa kitalu nyumba.
- Kuhamasisha ujenzi wa greenhouse (vitalu nyumba) **100** kufikia mwaka **2023** kupitia vikundi vya vijana au watu binafsi hususani waliopatiwa mafunzo ya kitalu nyumba.
- Kuhamasisha na kutoa elimu juu ya uanzishwaji wa viwanda vidogovidogo vya kuchakata mazao ya bustani

Kwa Mawasiliano zaidi;

- Wasilia na Afisa Kilimo aliyepo karibu na eneo lako AU
- Maafisa Kilimo waliopo katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kupitia Namba za simu

**+255753834085, +255762
191293,+255768537925 na
+255755653003**

Mawasiliano haya yatakusaidia

- Endapo kama utahitaji elimu ya Kitalu Nyumba (greenhouse) AU
- Kujengewa Kitalu Nyumba cha kwako wasiliana na watalaam kwa namba zilizopo hapo juu.

OFISI YA MKUU WA MKOA RUVUMA,

Simu Na: 2602256/2602238

Fax Na: 2602144

Anwani ya Posta: S.L.P. 74, Songea
Email: ras.ruvuma.@tamisemi..go.tz
aeaps@ruvuma.go.tz



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKAL ZA MITAA

Kilimo cha Teknolojia ya Kitalu Nyumba (Greenhouse)



*Picha ya kitalu Nyumba ya miti iliyojengwa Songea Manispaa
Eneo la Seed Farm.*

MKOA WA RUVUMA



KILIMO CHA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA KITALU NYUMBA (GREENHOUSE) NA FAIDA ZAKE.

A. Utangulizi.

Nini maana ya Kitalu Nyumba/ Greenhouse; hii ni Teknolojia inayotumika kuzalishia mazao kwa kutumia jumba lili- lojengwa kwa vifaa maalum.

B. Aina za Kitalu Nyumba/Greenhouse zimega wanyika kulingana na;

1. Kigezo cha umbile la Kitalu Nyumba
2. Kigezo cha matumizi;
 - Matumizi ya joto
 - Matumizi ya Baridi
3. kigezo cha vifaa au matengenezo
 - Za miti (wooden frame frame Structure)
 - Za kutumia mabomba(pipe frame structure)



- Za kutumia Vyuma(Aluminium frame structure
4. kigezo cha zana za ufunikaji (Covering type)
 - Za kutumia / kufunikwa na vioo (glass greenhouse) or Screenhouse) aina hii inatumika sana maeneo yenye baridi kali
 - Za kutumia/ kufunikwa na plastic (Polythene Sheet / plastic Film.
 5. kigezo cha gharama ya kitalu Nyumba

C.Faida za Kilimo cha Teknolojia ya Kitalu Nyumba (Greenhouse)

- Kuzalisha mazao mengi katika eneo dogo.
- Kuzalisha mazao yenye ubora zaidi.
- Uwezo wa kudhibiti hali ya hewa (micro climate) ndani ya greenhouse hatimaye kutengeneza maz- ingira mazuri ya ukuaji wa mimea.
- Kumwezesha Mkulima kuzalisha wakati wowote, kwa kuwa kitalu nyumba hutumia kilimo cha um- wagiliaji.
- Kupunguza matumizi ya viwatilifu, sababu ya mazao kuwa ndani ya Kitalu Nyumba (greenhouse) hivyo uvamizi wa visumbufu vya mimea ni kidogo.
- Kupunguza matumizi ya mbolea za viwandani, na kutumia mbolea ya samadi kwa kiasi kikubwa.
- Kupunguza kiasi kikubwa cha matumizi ya maji kwani umwagiliaji hufanyika kwa njia ya matone (drip irrigation), ambapo maji yanaenda moja kwa moja kwenye shina la mmea.

D. Gharama ya ujenzi wa Kitalu Nyumba

- Ya chuma yenye ukubwa wa mita 8 kwa mita 30 ni milioni 15 pamoja na gharama za ufundi
- Ya miti yenye ukubwa wa mita 8 kwa mita 30 ni milioni 6 pamoja na gharama za ufundi

E. Uzalishaji wa mazao (Nyanya) katika eneo la ukubwa wa mita 8 kwa mita 30.

- Idadi ya miche ni **700**
- Mche mmoja unazaa kilo **20-25**
- Mazao yanavunwa kwa miezi sita mfululuzo
- Kwa idadi ya miche **700** ni sawa na kilo **1400-17500** sawa na tani **14-17.5**
- Kwa bei ya T.sh 1,000 kwa kilo ni sawa na T.sh **14,000,000 - 17,500,000**
- Ili kupata bei nzuri ya mazao (Nyanya) zalisha msimu wa mvua. Kwa Ruvuma kuanzia mwezi wa **12 - 06.**

F.Aina ya Mazao yanayoweza kuzalishwa kwa kutumia Teknolojia ya Kitalu Nyumba (Greenhouse).

Kitalu Nyumba ni Kilimo chenye gharama kwa maana ya uanzishaji wake (Initial Cost) ukilinganisha na kilimo cha kawaida. Hivyo Mkulima anatakiwa kulima mazao yenye thamani ili kumfanya aweze kupata kipato kikubwa kama vile;

Nyanya, pilipili, Hoho, matikiti maji, matango, maua, kuotesha miiche kama vile; miiche ya kahawa, korosho nk.

Picha ya greenhouse ikionesha zao la nyanya.



•

Matumizi ya viuatilifu kuwadhibiti husababisha madhara kiafya kwa mlaji kupitia mazao ya mimea (Phytotoxicity)